

## JINSI YA KUVUNA

Vuna wakati mbaazi zimekomaa vizuri vitumba vinapobadilika kuwa na rangi ya kahawia. Vuna kila baada ya siku 3 hadi 5 kwa kuchuma vitumba au kukata matawi. Kausha juani, piga na kupeta.



Mbaazi iliyokomaa tayari kwa kuvunwa

## KIASI CHA MAVUNO

Mbaazi za muda mfupi hutoa kilo 600-800 (magunia 6-8) kwa ekari au kilo 1500-2000 kwa hekta kama zimetunzwa kwa kufuata maelekezo yaliyomo humu.

## KUHIFADHI

Baada ya kupeta, weka kwenye vyombo safi visivyokuwa na wadudu au;

- Tumia kiuwadudu cha maji cha Actellic 50EC,
- Hifadhi bila kutumia kemikali kwa njia ya mifuko ya PICS.
- Changanya kipaketi cha gramu 200 cha kiuwadudu shumba katika ma gunia mawili ya kilo mia (100kg) ya mbaazi.

Jinsi ya kutengeneza mafuta ya muarobaini.

- Pasua mbegu za muarobaini.
- Peta kuondoa uchafu na maganda.
- Twanga mbegu ilizilaiinike kama ngumu nyunyiza maji.
- Ongeza maji kidogo kisha kamua. Kwa njia hii unaweza kupata glasi moja ya mafuta kutoka kwenye kilo moja ya mbegu.
- Changanya glasi moja ya mafuta kwa kilo 100 za mbaazi.

## UPATIKANAJI WA MBEGU


Mbegu za awali za muda mfupi zinapatikana katika Kituo cha Utafti wa Kilimo llonga na mbegu za msingi zinapatikana kwa wakala wa mbegu za kilimo (ASA).

## Kwa maelezo zaidi pamoja na

### mahitaji ya mbegu wasilianana na:

Mkurugenzi wa Kanda, Utafti na Maendeleo Kanda ya Mashariki,  
Kituo cha Utafti wa Kilimo, ILONGA,  
Sanduku la Posta 33, Kilosa, Tanzania  
Simu: 023 2623201  
Fax: 023 2623284  
Barua pepe: [ilonga.ari@gmail.com](mailto:ilonga.ari@gmail.com)

# KILIMO BORA CHA MBAAZI ZA MUDA MFUPI



## Kimetayarishwa na:

Kituo cha Utafti wa Kilimo, ILONGA,  
Sanduku la Posta 33, Kilosa, Morogoro,  
Simu: 023 2623201  
Nukushi: 023 2623284  
Baruapepe: [ilonga.ari@gmail.com](mailto:ilonga.ari@gmail.com)

©Chapisho la Utafti wa Kilimo Kanda ya Mashariki - ARI llonga

**TOLEO 2016**

Uchapishaji umegharamiwa na Mradi wa AGRA



## **KILIMO BORA CHA MBAAZI ZA MUDDA MFUPI**

### **UTANGULIZI**

Mbaazi za muda mfupi hukomaa kati ya siku 120 hadi 125 katika maeneo ya Morogoro, Tanga, Pwani, Mtwara na Dar-es-salaam. Katika ukanda wa juu kwenye baridi, mbaazi za muda mfupi hukomaa kwa muda mrefu zaidi ya siku 120. Mbaazi za asili hukomaa kati ya siku 210 hadi 270. Mbaazi za muda mfupi hutoa mavuno mengi zaidi ya zile za asili iwapo zitalinwa kwa kuzingatia maelezo ya kitaalamu.

### **FAIDA ZA MBAAZI**

Mbaazi ni zao la jamii ya mikunde, faida kubwa za zao hili ni:

- Chanzo cha viini lisho vya protini kwa binadamu na wanyama
- Linavumilia ukame
- Hupunguza umasikini kwani zao hili ni chanzo cha mapato kwa kaya
- Hurutubisha udongo

Ili kujipatia mazao mengi na bora ya mbaazi za muda mfupi zingatia maelezo yaliyomo kwenye kipeperushi hiki.

## **AINA**

Mbaazi aina ya Komboa imefanyiwa utafti na kutolewa katika kituo cha Utafti Ilonga, Kilosa na kuonekana bora.

### **WAKATI WA KUPANDA**

Mbaazi za muda mfupi zinaweza kupandwa wakati wa masika au mvua za vuli za kuaminika katika ukanda wa Pwani.

### **NAFASI YA KUPANDA**

Panda kwa umbali wa sentimita 50 kati ya mistari na sentimita 20 kati ya mashina. Panda mbegu 3 kila shimo. wiki mbili baada ya kuota, punguza mmea mmoja ili ibaki miwili kwa kila shina. Ili kupanda heкта moja unahitaji wastani wa kilo 20 za mbegu ya mbaazi za muda mfupi ambayo ni sawa na kilo 8 kwa ekari. Usichanganye na mazaao mengine.

### **PALIZI**

Hakikisha shamba linakuwa safi kwa kupalilia mara kwa mara katika wiki 6 za mwanzo. Baada ya hapo palilia tu inapobidi kufanya hivyo.

### **UDHIBITI WA WADUDU**

Mbaazi za muda mfupi hushambuliwa sana na wadudu. Nyunyiza kiuwadudu mara tu zinapoanza kutoa maua, rudia kunyunyiza kila baada ya siku 10 hadi

kukomaa. Viuwadudu vinavyofaa ni Karate, Amerate, Profecron, COLT (chlorpyrifosi), au nyingine utakayoshauriwa na mtaalamu wa kilimo.



*Unyunyiziwi wa kiuwadudu shambani*

### **Jinsi ya kuchanganya viuwadudu**

- Changanya 40cc za karate katika lita 15 za maji au 40cc katika ULVA kwa lita moja ya maji au
- Changanya 40cc za Amerate SEC katika lita 15 za maji au
- Changanya 40cc za Profecron katika lita 15 za maji au
- Changanya 40cc za COLT (chlorpyrifosi) katika lita 15 za maji na kisha nyunyiza shambani.